

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

Simuyamdomo: 027 2977402

Tel Fax: 027 2977402

Email: ded@handenidc.go.tz

Tovuti: www.handenidc.go.tz



Ofisiya Mkurugenzi
Mtendaji (W)
S.L.P. 355,
Handeni
Tanga,

TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI .

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imepongeza na kutoa zawadi kwa shule kumi za Msingi na moja Sekondari kwa kufanya vizuri kwenye mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne mwaka 2016. Zawadi hizo zilitolewa kwenye kilele cha maadhimisho ya juma la elimu yaliyofanyika kiwilaya Wilayani Handeni kwenye shule ya Msingi Kabuku nje.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo Mkuu wa Wilaya ya Handeni ambaye pia alikuwa mgeni rasmi Mh. Godwin Gondwe aliwapongeza walimu na wadau wengine wa elimu kwa kazi nzuri wanazofanya na wanazoendelea kufanya katika kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora.

“elimu ni ufunguo wa maisha na kwamba Handeni hakuna mtoto mjinga, wazazi na walezi himizeni watoto kutumia fursa ya Elimu bure inayotolewa na Raisi wa Tanzania” Alisema.

Aidha ameeleza kuwa atahakikisha fedha zinazohusu madai ya walimu zinapofika Halmashauri zinawafikia walengwa kwa wakati uliopangwa. Aliwataka wakuu wa shule na Maafisa elimu Kata kusimamia haki ya msingi ya wanafunzi kupata elimu wanayostahili.

Wakati huohuo amepiga marufuku watoto walio na umri wa kuwepo shulenii kuacha kuchunga mifugo hasa kwa siku za shule baada ya kubainika watoto wengi wa jamii ya wafugaji wanatumiwa kuchunga mifugo badala ya kwenda shule. Amewaonya wazazi na jamii ya wafugaji ambao wanakwamisha watoto kupata haki yao ya msingi ya kupata elimu na kwamba sheria itachukua mkondo wake kwa yejote atakayebainika kwenda kinyume. Amewaeleza pia wazazi ambao wanawatoto waliovuka umri wa kwenda shule kupelekwa kwa utaratibu wa MEMKWA.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Bw. William Makufwe ,amesema kuwa kukosekana kwa chakula cha kutosha shulenii, utoro uliokithiri kwa baadhi ya wanafunzi, kutokujibika kwa baadhi ya walimu na wazazi pamoja na upungufu wa walimu kunasababisha kwa kiwango kikubwa kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi.

Ameagiza shule ambazo mpaka sasa ambazo hazina chakula kuhakikisha wanawapa wanafunzi chakula. Aliwataka pia kusimamia mazao ya mihogo waliyopanda ili mazao hayo yaweze

kusaidia upatikanaji wa chakula shulenii na kuongeza kiwango cha uelewa kwa wanafunzi. Ametoa mwezi mmoja hadi kufikia 4/5/2016 kwa Maafisa watendaji Kata, Vijiji, walimu wakuu, wakuu wa shule na Maafisa elimu Kata kuhakikisha kuwa watoto wanapata chakula cha mchana shulenii.

Shule za Msingi zilizopata zawadi na pongozi ni Tewe iliyokuwa ya sita kimko na kuzawadiwa Tsh. 200,000/=, Chang'ombe Tsh. 150,000/=, Mkumba Tsh 100,000/=, Mzundu Tsh. 82,000/=, Kwaragulu , Mbwewe, Kwamdani, Kwedikwazu Magharibi, Kwedikwazu Mashariki na chogo ambazo zote zilipata Tsh 78,000/. Mazingara sekondari imepata zawadi Tsh.100000/=.

Alda Sadango
Afisa Habari
Halmashauri ya Wilaya Handeni.